# NYERI COUNTY
# DARASA LA SABA MUHULA WA TATU

PENPLUS KIRINYAGA

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

1. *Tumia penseli ya kawaida.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:*
   *(I) JINA LAKO* *(II) JINA LA SHULE YAKO*
3. *Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.*

---

***Chagua jibu sahihi kwa yale uliyopewa kujazia nafasi iliyoachwa wazi.***

Watu wengi husadiki kwamba watoto ___1___ hufuata ___2___ ya wazazi wao. Mzazi akiwa na ___3___ njema, pana ___4___ watoto wawe ___5___ hivyo kwani wahenga ___6___ mwana hutazama kisogo cha ___7___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. huleta | B. husadiki | C. aghalabu | D. huapa |
| **2.** | A. mielekeo | B. miendo | C. mwenendo | D. nyayo |
| **3.** | A. kazi | B. hulka | C. sura | D. nia |
| **4.** | A. uwezekano | B. uwezo | C. tetezi | D. ukweli |
| **5.** | A. hivyo | B. vile | C. hivi | D. vivyo |
| **6.** | A. waliamba | B. walighilibu | C. walihadaa | D. walitambaa |
| **7.** | A. dadake | B. ninake | C. babake | D. nduguake |

Timu ___8___ shule yetu ___9___ imefanya mazoezi ___10___ kutosha na ilikuwa tayari ___11___ na ___12___ washindi . Tulipofika uwanjani, tulikuta ___13___ wamejaa wakingoja ___14___ ziumizwe. Tulishangilia kwa vifijo na ___15___ za furaha.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | A. za | B. la | C. wa | D. ya |
| **9.** | A. zilikuwa | B. lilikuwa | C. ilikuwa | D. walikuwa |
| **10.** | A. za | B. ya | C. vya | D. kwa |
| **11.** | A. kushindana | B. kutazamana | C. kukaribiana | D. kushikana |
| **12.** | A. kuipuka | B. kuibuka | C. kutokea | D. kupata |
| **13.** | A. wakimbiaji | B. wanasoka | C. mashabiki | D. wasafiri |
| **14.** | A. nyazi | B. nyasi | C. uamuzi | D. kuta |
| **15.** | A. deremo | B. nderemo | C. ndelemo | D. delemo |

16. ***Jibu swali kinyume cha neno lenye kistari chini yake.***

Badala ya <u>kutabasamu</u> alianza________

A. kulia B. kucheka

C. kununa D. kuruka

17. Ni nini ukubwa wa sentensi hii.

**Mbwa mweusi ameangukia mti.**

A. Kijibwa cheusi kimeangukia kijiti.

B. Jibwa leusi limeangukia jiti.

C. Kijibwa mweusi kimeangukia mti.

D. Jibwa jeusi limeangukia jiti.


18. Tumia kivumishi mwafaka kwa kujazia pengo

**Nilinunua fagio _____ sokoni.**

A. mbili B. bili

C. mbiri D. mabili

19. Umbo hili ni



A. kopa B. roho

C. duara dufu D. pia

20. Ndugu wa kike wa mama huitwaje?

A. Shangazi B. Mjomba

C. Halati D. Hau

21. ***Andika kwa tarakimu.***

Humusi tatu

A. $^5/_3$ B. $^1/_7$

C. $^3/_9$ D. $^3/_5$

22. Kutokana na jina uashi tutapata kitenzi

A. Aka B. Asi

C. Ashi D. Mwashi

23. Bainisha sentensi inayoonyesha kivumishi kimilikishi.

A. Gari hili ni jipya

B. Nyumbani kwako ni kuzuri.

C. Alifurahi bali hakucheka.

D. Mtoto mtiifu hupendeza.

24. ***Kanusha sentensi uliyopewa.***

Mwalimu afundishaye ni mwema.

A. Mwalimu afundishaye si mwema.

B. Mwalimu anayefundisha si mwema.

C. Mwalimu asiyefundisha si mwema.

D. Mwalimu afundishaye ni mbaya

25. Mtu anayebeba mizigo kwa kulipwa huitwaje?

A. Kuli

B. Utingo

C. Machenga

D. Hamali

26. Ni sentensi ipi iliyoonyesha matumizi ya kwa_____

A. alienda kwa chumba.

B. alienda kwa shule.

C. tulifika kwa wakati.

D. walilembea kwa mamake hadi sokoni.

27. ***Kamilisha methali hii.***

Ganda la mua la jana chungu kaona__________

A. chakula B. kivuno

C. makazi D. kinywaji

28. Andika kisawe cha barabara.

A. baraste B. ndezi

C. wajihi D. chichiri

29. Neno wavu liko katika ngeli ya_____

A. A- WA B. I - ZI

C. U - I D. U - ZI

30. Silabi moja katika shairi huitwaje?

A. Kibwagizo

B. Mloto

C. Mzani

D. Kina

***Soma kifungu hiki kisha uchague majibu sahihi zaidi kujazia na kwa maswali uliyopewa.***

Mlango ulibishwa kwa upole mara ya kwanza na ya pili. Mara ya tatu mke akanyanyuka kutaka kwenda kuufungua. Papo hapo mume akamnong'onezea, 'Ngojea bibi wee! Ngoja nifiche chakula hiki mvunguni. Kuku huyu ninavyomtamani siwezi kumgawia mwingine. Hawa ni hao watu wasiojua desturi wala mila. Vipi wanamwendea mtu nyumbani kwake saa hizi za maakuli ya chajio?

Bibi hakuyafurahia yaliyosemwa lakini hakuwa na la kufanya ila kutii amri. Baada ya mume kuficha chakula mvunguni, bibi akaufungua mlango, mameno ya mume hayakuanguka. Ni maskini aliyekuwa akiomba chakula. Aliyejibu ni mume. "Sisi watuona tumepakata mikono hatujaraba riziki hata staftahi hatukuiona, usituzidishe dhiki tulizonazo."

Miaka, kapita. Bibi huyu akashindwa kuvumilia tabia ya mumewe. Mume akamtaliki na baada ya miaka kadhaa akaolewa na mume mwingine. Bwana aliyemwoa alikuwa tofauti kabisa na bwana yake wa kwanza. Hata siku moja mlango ukabishwa. Walikuwa wanataka kula chamcha. Mke akasita kwenda kuufungua malango mume akamhimiza aende kuufungua mlango. Kumbe ni maskini aliyeomba chakula. Mke hakujua la kujibu maana yu mgeni kwa mume huyo wa pili aliyekuwa naye. Bwana akamwamuru mke ampatie nusu ya chakula chao na kumtilia katika sufuria. Maskini alishukuru sana na kuwaaga. Punde tu alipotoka, mke akaanza kulia. Mume hakufurahi kumwona mkewe anabubujikwa na machozi.

"Mbona unalia" mke akasema "yule maskini ni mtalaka wangu. Siku moja alikuja maskini kuomba chakula. Akaficha na kumkaripia ajabu. Leo ni yeye anayeomba ukampa zaidi ya alichotarajia na maneno matamu juu.

Mume akasema, "Na mimi ndiye yule maskini aliyekaripiwa. Niliona sura yako ilivyokunjika nilipokaripiwa. Mungu aliponiyua umaskini nikakutafuta na kukuoa.

---

**31.** Waliohusika ni wangapi katika mkasa huu?
A. 5 B. 3 C. 2 D. 4

**32.** Mlango ulibishwa mara ngapi?
A. 3 B. 2 C. 5 D. 4

**33.** Mume alificha chakula wapi?
A. Kabatini
B. Chumbani cha kulala
C. Chini ya kitanda
D. Chini ya meza.

**34.** Kulingana na kisa hiki, mume wa kwanza alikuwa____
A. mkarimu B. mstahimilivu
C. mbishi D. bahili

**35.** Chajio ni chakula cha ____
A. usiku B. asubuhi
C. mchana D. alfajiri

**36.** Kwa nini mke alisita kuufungua mlango mara ya pili?
A. Aliogopa maskini
B. Mume alikuwa na wivu
C. Hakujua tabia ya mume wa pili
D. Alikuwa amechoka

**37.** Kilichomfanya mke kulia ni nini?
A. Maskini kuomba chakula.
B. Kuona maskini mtalaka wake.
C. Maskini alivyovalia.
D. Chakula kupungua.

**38.** Mke alibubujikwa na machozi____
A. kwi kwi kwi
B. ji
C. puku puku
D. zi

**39.** Kwa nini mume alimzuia mkewe kuufungua mlango?
A. Hakutaka wageni
B. Alitaka kuficha chakula kwanza.
C. Alikuwa na chakula kingi
D. Alitaka kumaliza chakula kwanza.

**40.** Methali mwafaka kwa kisa hiki ni ____
A. usipoziba ufa utajenga ukuta.
B. maskini akipata makalio hulia mbwata.
C. cheza na mwenye mali usicheze na mali
D. dunia mwendo wa ngisi

---

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50***

Ukiyasoma majarida mbalimbali utazipata takwimu za kushangaza. Nyingi za takwimu hizi zinasababisha mtu hata akose matumaini. Takwimu zinaonyesha kuwa, watoto wanaokufa kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano bado ni wengi. Wafao wakati wa kuzaliwa bado ni tele. Watu waambukizwao virusi vya ukimwi kila dakika ni wengi. Watu wanaokufa mikononi mwa majambazi wanazidi kuongezeka nao wafao katika ajali barabarni, si haba watoto wetu wa kike wanaobakwa na wanyama katika ngozi za binadamu, idadi yao inazidi kuongezeka kila kukicha.

Utazidi kupoteza matumaini ukisoma na usikie kuwa vijana wetu wanazidi kujiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya na pia vitendo vya ngono. Takwimu za watoto wafao kutokana na maradhi ya malaria nazo zinatisha. Si semi wafao kwa maradhi mengine kama vile kifaduro, ifahamike kuwa, wengine hufa kutokana na utapi wa mlo.

Upande wa uchumi, hakuna habari njema vilevile. Bila shaka kufikia sasa umezoea kusikia kuwa, zaidi ya sudusi ya raia nchini wamo katika kitovu cha umaskini. Hawawezi kupata hata angalau shilingi themanini kwa siku.

Hebu fikiria kuhusu kiongozi wa jamii aliye na watoto sita ilhali hawezi kupata angaa shilingi themanini kwa siku. Nafasi za ajira nazo ni haba idadi ya wasio na kazi wala bazi inazidi kuongezeka.

Kulingana na takwimu hizo, lile linaloonekana kukua kwa haraka ni mitaa ya mabanda katika miji yetu. Na, je, unaelewa kuwa zaidi ya aislimia sabini ya wakazi wa mingi ya miji yetu huishi mitaa ya mabanda? tafadhali lifikirie hilo.

Nalo pengo kati ya matajiri na maskini linazidi kushamiri , matajiri wanazidi kunawiri huku maskini wakiendelea kudidimia na wengine hata kufifia kabisa.

Hali ya mazingira haijaonyesha lolote la kuinua nyoyo zetu. Takwimu zinazidi kuonyesha misitu yetu inazidi kuangamizwa. Mito nayo inazidi kukauka. Maziwa yetu yanazidi kukauka na kuchafuka. Navyo viumbe vya majini vinazidi kufariki dunia. Inasemekana pia kiwango cha joto duniani kinazidi kuongezeka. Si ajabu kuikosa theleji kilele mwa mlima Kenya miaka michache ijayo. Nayo maradhi ya ngozi na ya saratani ya ngozi yazidi kuathiri na kufilisi ndugu na wazazi wetu.

Swali ni, je tunaelekea wapi? Je, mambo haya yanatokea kwa kuwa hatuna uwezo wa kuyadhibiti au ni kwa sababu tunayavalia miwani? Katu, siamini kuwa hatuwezi kuyashinda. Uwezo tunao lakini nia haipo. Pasipo nia, njia haipo. Lakini tumaini lipo. Si tumaini pekee. Hata suluhisho. Nayo hayo ya mikononi mwenu enyi vijana. Kumbukeni mnao uwezo. Ni nyinyi viongozi wa kesho. Someni kwa bidii, mwajibike ili muinusuru dunia .

---

**41.** Katika aya ya kwanza, mwandishi ameyataja majanga mangapi?

A. Sita B. Saba C. Matano D. Manne

**42.** Kulingana na kifungu, mbali na maradhi watoto wachanga aidha wanatishwa na___

A. ukimwi
B. dawa za kulevya
C. ukosefu wa chakula
D. wizi

**43.** Ni maelezo yapi sahihi.

A. Ugonjwa wa malaria huwakumba watoto pekee.
B. Vijana wetu wametupilia mbali ouvu wa ngono.
C. Kifaduro ni uwele uwatishao watoto.
D. Mengi ya maradhi yanadidimia.

**44.** Kwa mujibu wa mwandishi, uhaba wa ajira unaweza kuzua matokeo yapi?

A. Uhalifu
B. Kuimarika kwa uchumi
C. Gharama ya maisha kupanda
D. Hutujaelezwa

**45.** Kwa mujibu wa mwandishi, saratani ya ngozi inasababishwa na______

A. lishe bora
B. mitaa ya mabanda
C. uchafuzi wa mazingira
D. manukato yenye kemikali hatari.

**46.** Je, unadhani hali ya mambo inayoelezwa hupatikana wapi?

A. Nchi zilizoendelea.
B. Ni vigumu kujua.
C. Katika mataifa yote duniani.
D. Ulimwengu wa tatu.

**47.** Kulingana na kifungu, ni takriban kiasi kipi cha wakazi wa mjini hakiishi katika mitaa ya mabanda?

A. Asilimia sabini B. Ushuri tatu
C. Asilimia kubwa D. Sudusi

**48.** Ni bayana kuwa uharibifu wa mazingira utasababisha?

A. Kuzuka kwa maradhi kama vile ukimwi.
B. Kuangamia kwa viumbe mbalimbali
C. Kuongezeka kwa viwanda.
D. Kupunguka kwa kiwango kati ya wakwasi na walalahoi.

**49.** Kulingana na taarifa, ni kipi kiini cha matatizo yote yaliyozungumziwa?

A. Ugumu wa maisha. B. Mazingira
C. Matendo ya binadamu D. Umaskini

**50.** Ni sahihi kusema kuwa ____

A. Mwandishi ni mkwasi wa mali.
B. tamaa ya mwandishi ya kushuhudia maisha bora imetamauka.
C. Vijana wana fursa na satua ya kuboresha mambo .
D. Binadamu hana uwezo wa kuyatatua matatizo yanayozungumziwa.